Pg 7. Mwananchi Jumatatu Mei 14 2026

# Madereva masafa marefu washukuru serikali kuwatambua, kuwathamini

Na Rehema Lugono

CHAMA cha Madereva wa Malori ya Masafa Marefu Tanzania (TLDTA) kimeishukuru serikali kwa kutambua kuwathamini madereva.

Mwenyekiti wa TLDTA, Hassan Dede alisema hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari Dar es Salaam jana.

"Serikali ya Awamu ya Sita kuanzia Rais Samia na wabunge wamekuwa wakituthamini kwa kushinikiza na kuboreshwa kwa mifumo ya mikataba ya kazi, kupunguzwa kwa gharama za ada ya leseni kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), vyuo vya usafirishaji pamoja na usimamazi mazingira salama yenye utu ya utendaji kazi kwa madereva wa masafa marefu na usafiri wa umma," alisema Dede.

Alisema hatua hiyo ni ukombozi wa maslahi yao kwa sababu inagusa mioyo ya madereva ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakipigania haki zao bila matokeo ya haraka.

Dede alisema sekta ya usafirishaji ni miongoni mwa nguzo kuu za uchumi wa nchi, hivyo kitendo cha Rais Samia na Bunge kuingilia kati na kuweka jicho katika ustawi wa madereva kitasaidia kupunguza migogoro ya kikazi na kuongeza ufanisi barabarani.

"Rais Samia ametufungulia mipaka ya nchi tumeshuhudia shehena za mizigo zikishuka bandarini ambazo ndio zinatupa ajira za kuipeleka mizigo hiyo kutoka sehemu moja kwenda nyingine," alisema.

Dede aliipongeza Wizara ya Uchukuzi kwa kwa kuweka miundombinu vizuri.

Alisema kwa mara ya kwanza chama hicho kimepata mwaliko wa kwenda bungeni kuhudhuria uwasilishaji wa bajeti.

Dede ametoa mwito kwa Watanzania kuendelea kudumisha amani ya nchi inayowezesha wananchi kufanya shughuli zao.